# MFALME MTUKUFU

## Wimbo wa katikati

JOHN SEBASTIAN






1.Nchi na vyote viijazavyo ni mali yake,
Dunia ameiweka wakaao ndani yake.
Maana ameiweka misingi yake juu ya bahari,
Na juu ya mito ya maji ameithibitisha.

2. Ni nani atakayepanda katika mlima wa Bwana,
Ni nani atakayesimama katika patakatifu pake.
Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe,
Asiyeiinua nafsi yake kwa ubatili.

3. Atapokea baraka kwa Bwana,
Na haki kwa Mungu wa wokovu wake.
Hiki ndicho kizazi cha wakutafutao,
Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa Yakobo.